MWONGOZO WA KUWASILISHA MAPENDEKEZO KWA AJILI YA MAPITIO YA SHERIA KWA TUME YA KUREKEBISHA SHERIA ZANZIBAR

Makundi/ Watu wanaoweza kuelekeza / kuwasilisha mapendekezo kwa ajili ya Mapitio ya Sheria

a) Waziri anayehusika na masuala ya Sheria;
b) Mwanasheria Mkuu;
c) Mahkama;
d) Wizara, Shirika la Serikali, Wakala wa Serikali au Taasisi ya Serikali inayojitegemea;
e) Taasisi binafsi au Jumuiya isiyo ya Kiserikali; au
f) Mwananchi yeyote.

Lugha ya Nyaraka:

Nyaraka zote zinazowasilishwa Tume kwa Sheria inayokusudiwa kurekebishwa, na nyaraka nyenginezo, zinapaswa kutayarishwa katika lugha ya Kiswahili. Taasisi itakayoona inafaa, inaweza pia kuleta nakala za nyaraka zikiwa katika lugha ya Kiswahili na kiingereza

Muda wa Kufanyia Kazi Mapendekezo

Mapendekezo maelekezo yanayohusu Utaratibu wa Kawaida

Mapendekezo yanayofikishwa mbele ya Tume ya Kurekebisha Sheria kwa utaratibu wa kawaida yatafanyiwa kazi, na Tume kukamilisha jukumu lake ndani ya muda usiozidi siku 45, hata hivyo muda huu unaweza kuzidi kwa kutegemea ukubwa wa kazi. Muda huu unahusisha mambo yafuatayo:

a) Kufanya utafiti wa awali wa Mapendekezo ya Sheria;
b) Kuandaa ripoti ya awali (inception report) kuhusu Mapendekezo hayo;
c) Kuwasilisha ripoti hiyo mbele ya Tume kwa mazingatio;
d) Kufanya utafiti
e) Kutafuta maoni kwa wananchi katika maeneo yao;
f) Kufanya mikutano na wadau wanaohusiana na Mapendekezo husika;
g) Kuandaa ripoti na kuiwasilisha katika vikao vya Tume kwa mazingatio
h) Kuwasilisha ripoti Serikalini (kwa waziri anayehusika na masuala ya Sheria)

Mapendekezo maelekezo katika hali ya dharura

Kwa Mapendekezo ya Mapitio ya Sheria yatakayojitokeza katika hali ya dharura ambayo yatahitaji kufanyiwa kazi kwa uharaka, Tume itafanyia kazi Mapendekezo hayo na kukamilisha jukumu lake ndani ya muda wa wiki tatu. Mapendekezo hayo yatafikishwa Tume ya Kurekebisha Sheria yakiambatana na Hati ya Serikali iliyosainiwa na Waziri anayehusika na masuala ya Sheria, inayothibitisha kuwa Mapendekezo hayo yanapaswa kuzingatiwa katika hali ya dharura. Aidha, Mapendekezo hayo yatazingatia nyaraka zilizoainishwa katika muongozo huu kama ni kwa ajili ya kupelekea kutungwa kwa Sheria mpya au kufanya mapitio ya sheria iliyopo, kadri itakavyokuwa.

MUHTASARI WA UWASILISHAJI WA MAPENDEKEZO

ASILI YA MAPENDEKEZO	WAJIBU WA WIZARA/TAASISI YA UMMA AU TAASISI NYENGINEZO	WAJIBU WA TUME
Mapendekezo yanayohitaji kufanyiwa utafiti kwa ajili ya Sheria mpya:	a) Kuwasilisha Kibali cha Serikali cha kuruhusu kutungwa kwa Sheria hiyo ikiwa Sheria hiyo inakusudia kuanzisha Taasisi mpya na hivyo kuathiri masuala ya kifedha; na b) Dhana ya Mapendekezo ya kutungwa kwa sheria mpya. Dhana hiyo inapaswa kujumuisha yafuatayo:- i) Uchambuzi wa wazo la kuwa na sheria mpya ukijumuisha changamoto za kisera na za	a) Kufanya utafiti kuhusiana na Mapendekezo Maelekezo yaliyofikishwa Tume hasa kuhusiana na mambo yafuatayo: i) Kama Mapendekezo hayo hayaendi kinyume na Katiba ya Zanzibar ya 1984 ii) Kama Mapendekezo hayo yapo katika mamlaka ya wizara au Taasisi husika ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar.

	kisheria ziliopo na zinazokusudiwa kuondolewa kwa kutungwa sheria ii) Maelezo kwa nini itungwe sheria mpya badala ya kufanyiwa marekebisho sheria iliyopo iii) Mapendekezo ya maeneo muhimu ya kuzingatiwa katika Sheria inayokusudiwa kutungwa kwa lengo la kuondosha changamoto ziliopo iv) Kuwasilisha sera zinazosimamia suala hilo linalohitaji kutungiwa Sheria mbele ya Tume kwa mapitio ya sera hiyo/hizo v) Uzoefu wa nchi nyengine za Ukanda wa Afrika Mashariki na maeneo mengine katika suala linalotaka kutungiwa sheria vi) Kuainisha Wadau muhimu wa kuzingatiwa wakati wa hatua za kutungwa kwa sheria mpya	iii) Kama Mapendekezo hayo hayapelekei mgongano baina ya Taasisi za umma. iv) Kama Mapendekezo hayo yana maslahi kwa umma (public interest) b) Kuandaa Taarifa ya Awali (Inception report) na kuiwasilisha katika kikao cha Makamishna wa Tume ya Kurekebisha Sheria kwa mazingatio na uamuzi c) Kufanya mapitio ya sera husika katika eneo linalotaka kutungiwa Sheria/ kurekebishwa Sheria d) Kufanya utafiti na mapitio ya Sheria inayopendekezwa kutungwa au kufanyiwa marekebisho e) Kuchukua maoni ya wananchi/wadau kadri inavyohitajika

	vii) Taaluma zinazohitajika katika hatua za utungwaji wa sheria hiyo mpya	f) Kuandaa taarifa na kuiwasilisha mbele ya kikao cha Makamishna kwa mazingatio na uamuzi g) Kuwasilisha taarifa Serikalini kupitia kwa Waziri anayehusika na mambo ya Sheria
Mapendekezo ya Kufanya Mapitio Sheria iliyopo:	i) Kibali cha Serikali cha kuruhusu kufanywa kwa marekebisho ya sheria ikiwa Mapendekezo hayo ya kurekebisha Sheria yanalenga kuanzisha Taasisi mpya au kubadili muundo wa Taasisi iliyopo na hivyo kuathiri masuala ya kifedha; na ii) Dhana ya mapendekezo ya kufanya marekebisho yanayokusudiwa. Dhana hiyo inapaswa kujumuisha yafuatayo:-	a) Kufanya utafiti kuhusiana na Mapendekezo yaliyofikishwa Tume hasa kuhusiana na mambo yafuatayo: i) i) Kama mapendekezo hayo hayaendi kinyume na Katiba ya Zanzibar ya 1984 ii) Kama Mapendekezo hayo yapo katika mamlaka ya wizara au Taasisi husika ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. iii) Kama Mapendekezo hayo hayapelekei mgongano baina ya Taasisi za umma.

	iii) Uchambuzi wa wazo la kufanya marekebisho katika Sheria iliyopo iv) Kuwasilisha sera zinazosimamia suala hilo linalohitaji kutungiwa Sheria mbele ya Tume kwa mapitio ya sera hiyo/hizo v) Changamoto ziliopo katika Sheria iliyopo zinazokusudiwa kuondolewa kwa kufanywa marekebisho ya sheria vi) Uzoefu wa nchi nyengine za Ukanda wa Afrika Mashariki na maeneo mengine katika suala linalohusu Marekebisho ya Sheria yanayokusudiwa kufanywa vii) Wadau muhimu wa kuzingatiwa wakati wa hatua	iv) Kama Mapendekezo hayo yana maslahi kwa umma (public interest) b) Kuandaa Taarifa ya Awali (Inception report) na kuiwasilisha katika kikao cha Makamishna wa Tume ya Kurekebisha Sheria kwa mazingatio na uamuzi c) Kufanya utafiti na mapitio kuhusiana na Sheria inayopendekezwa kutungwa au kufanyiwa marekebisho d) Kuchukua maoni ya wananchi/wadau kadri inavyohitajika e) Kuandaa taarifa na kuiwasilisha mbele ya kikao cha Makamishna kwa mazingatio na uamuzi f) Kuwasilisha taarifa Serikalini kupitia kwa Waziri anayehusika na masuala ya Sheria

	za kufanywa kwa marekebisho ya Sheria iliyopo viii) Taaluma zinazohitajika katika hatua za marekebisho hayo ya sheria	
Mapendekezo / maelekezo ya dharura katika kufanya tafiti kwa ajili ya Sheria mpya au mapitio Sheria iliyopo	ii) Kuwasilisha mbele ya Tume, Kibali cha Serikali cha kuruhusu kutungwa kwa Sheria mpya au kufanyiwa marekebisho sheria iliyopo, ikiwa Sheria hiyo inakusudia kuanzisha Taasisi mpya na hivyo kuathiri masuala ya kifedha; na iii) Kuwasilisha Dhana ya Mapendekezo kwa ajili ya kufanywa utafiti ili kutungwa kwa Sheria mpya au kufanya marekebisho katika sheria	a) Kufanya utafiti kuhusiana na Mapendekezo maelekezo yaliyofikishwa Tume hasa kuhusiana na mambo yafuatayo: i) Kama mapendekezo hayo hayaendi kinyume na Katiba ya Zanzibar ya 1984 ii) Kama Mapendekezo hayo yapo katika mamlaka ya wizara au Taasisi husika ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. iii) Kama Mapendekezo hayo hayapelekei mgongano baina ya Taasisi za umma.

	iliyopo. Dhana hiyo inapaswa kujumuisha yafuatayo:- i. Uchambuzi wa wazo la kuwa na Sheria mpya au kufanya marekebisho katika sheria iliyopo ukijumuisha changamoto za kisera na za kisheria ziliopo na zinazokusudiwa kuondolewa kwa kutungwa Sheria ii. Mapendekezo ya maeneo muhimu ya kuzingatiwa katika Sheria inayokusudiwa kutungwa au kurekebishwa kwa lengo la kuondosha changamoto ziliopo iii. Kuwasilisha sera zinazosimamia suala hilo linalohitaji kutungiwa Sheria/kurekebishwa sheria	iv) Kama Mapendekezo hayo yana maslahi kwa umma (public interest) b) Kufanya mapitio ya sheria inayopendekezwa kutungwa au kufanyiwa marekebisho c) Kuchukua maoni ya wananchi/wadau kadri itakavyowezekana d) Kuandaa taarifa na kuiwasilisha mbele ya kikao cha Makamishna kwa mazingatio na uamuzi e) Kuwasilisha taarifa Serikalini kupitia kwa Waziri anayehusika na mambo ya Sheria

	mbele ya Tume kwa mapitio ya sera hiyo/hizo iv. Wadau muhimu wa kuzingatiwa wakati wa hatua za kutungwa kwa sheria mpya kurekebishwa Sheria hiyo.	